

# CareerForce ni nini?

CareerForce ni rasilimali ya Minnesota inayolinganisha maendeleo ya kazi na talanta. Tuna washirika wengi wa kujumuika katika jimbo lote na kwa pamoja tumejitolea kutoa matokeo mazuri kwa watafutaji wa kazi, waajiri, jumuiya na kwa Minnesota. Mtu yeyote anaruhusiwa kupata programu na huduma zetu nyingi za ubunifu katika maeneo ya CareerForce katika jimbo lote au kwenye **CareerForceMN.com**.

# ANWANI YA

## mawasiliano


**Usaidizi wa Marekebisho ya Biashara (Trade Adjustment Assistance, TAA)**
Minnesota Department of Employment and Economic Development (Idara ya Ajira na Maendeleo ya Uchumi ya Minnesota)

1st National Bank Building
332 Minnesota Street, Suite E200
St. Paul MN 55101

Simu: 1-888-234-1330
au 651-259-7543
Barua pepe: deed.taa@state.mn.us

**CareerForceMN.com/TAA**


# TEMBELEA

## CareerForceMN.com/TAA
kwa maelezo zaidi

Kwa ombi, habari hii inaweza kupatikana katika miundo mbadala kwa watu wenye ulemavu.

CareerForce maeneo ya Minnesota ni waajiri na watoa huduma wa fursa sawa.

CareerForce ni mshirika anayejivunia kujumuika na Kituo cha Kazi cha Amerika (American Job Center).


08/2020 | Qty 2,000 DEED-01981-04


CareerForce™

*Minnesota's Career Resource*



# Kurudi Kazini Baada ya Kuachishwa Kazi Kuhusiana na Biashara

**Usaidizi wa Marekebisho ya Biashara (Trade Adjustment Assistance, TAA)**

# KURUDI KUFANYAKAZI

## na Huduma za Usaidizi wa Marekebisho ya Biashara



Programu ya Usaidizi wa Marekebisho ya Biashara (Trade Adjustment Assistance, TAA) ni mpango wa shirikisho ambayo hutoa misaada kwa wafanyikazi waliopoteza kazi zao, wako katika hatari ya kupoteza kazi zao, au ambao masaa yao ya kazi na mshahara imepunguzwa kutokana na ushindani wa kigeni.

Huduma za TAA zimeundwa kukusaidia kupata tena ajira ambayo ni sawa au bora kuliko kazi ambayo uko katika hatari ya kupoteza au tayari umepoteza.

### TAA, KWA KUSHIRIKIANA NA PROGRAMU YA MFANYAKAZI ALIYEONDOLEWA, INAWEZA KUTOA

**Huduma za Kuajiriwa Tena**

- Ushauri wa Ajira
- Tathmini ya Ujuzi na Hamu
- Utafutaji wa Kazi, maombi ya kazi, na warsha za kuhoji
- Huduma za Kutafuta Kazi kwa Kujielekeza

**Posho ya Utafutaji wa Kazi**
Kwa gharama zinazohusiana na kuhamia kwa kazi nje ya eneo lako

**Posho ya Uhamaji**
Kwa gharama zinazohusiana na kuhamia kwa kazi nje ya eneo lako

**Huduma za Mafunzo**
Wafanyikazi wanaostahiki wanaweza kuchagua moja ya chaguzi zifuatazo za mafunzo ndani ya muda maalum:

- Mafunzo ya darasani/mkondoni (fupi au ya muda mrefu)
- Mafunzo ya kazini
- Ukurufunzi/Mafunzo ya kutolewa na mwajiri

Mafunzo ya darasa yanaweza kujumuisha:

- Masharti zinazohitajika kwa programu iliyoidhinishwa ya mafunzo
- Kozi zinazomatokeo ya shahada, digrii, diploma, au sifa inayotambuliwa kwa sekta

**Posho ya Marekebisho ya Biashara (Trade Readjustment Allowance, TRA)**
Misaada za kupanuliwa kwa ukosefu wa ajira kwa wafanyikazi wanaostahiki waliojiandikisha katika mafunzo ya wakati wote yaliyoidhinishwa na TAA

**Posho ya Usafiri na ya Kujikimu**
Kwa gharama za kuhudhuria mafunzo nje ya eneo lako

**Usaidizi wa Marekebisho ya Biashara ya Ajira Mpya (Reemployment Trade Adjustment Assistance, RTAA)**
Nyongeza ya mshahara inapatikana kwa wafanyikazi wenye umri wa miaka 50 au zaidi ikiwa kazi mpya inalipa chini ya cheo chao iliyoathiriwa na biashara

**Mkopo wa Ushuru wa Bima ya Afya (Health Coverage Tax Credit)**
HCTC hulipa asilimia 72.5 ya ada zinazostahili za bima ya afya kwa watu wanaostahiki na familia zao; inasimamiwa na IRS

Tembelea **CareerForceMN.com/TAA** kupata maelezo zaidi kuhusu huduma za TAA

# TAA

## Mchakato wa Kuidhinisha Maombi

1. **Biashara inafunga, inatishia kufutwa kazi, au inafuta wafanyakazi.**
2. Kikundi cha wafanyikazi watatu au zaidi, afisa wa kampuni, mwakilishi wa chama cha wafanyakazi, au mshirika wa CareerForce **anawasilisha ombi kwa Ofisi ya Idara ya Kazi ya Amerika ya Usaidizi wa Marekebisho ya Biashara (U.S. Department of Labor's Office of Trade Adjustment Assistance, OTAA)**.
3. **OTAA inachunguza ombi.**
4. **OTAA inathibitisha au kukataa ombi la kustahiki kwa TAA.**

# HATUA ZAKO ZIFUATAZO

1. **Ikiwa ombi limethibitishwa, TAA itakutumia barua ya kustahiki na Kijitabu cha Mwongozo ya TAA kupitia barua ya kutoa uhakikisho.**
2. **Husiana na Mtoa huduma ya Mfanyakazi Aliyeondolewa ili kuanza;** kila huduma ya TAA ina ratiba yake yenyewe. Watoa huduma wanaweza kupatikana: mn.gov/deed/job-seekers/recently-unemployed/layoff/dwp-service-providers.jsp